

## **LEARNING BY EAR 2012**

**“Bado ningali mwanadamu – Riwaya inayoangazia matatizo  
wanayopata wauguaji wa maradhi ya akili barani Afrika”**

### **EPISODE 6: “Hakuna la rahisi”**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**

**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

#### **SCENE ONE: DORA NA IRENE WAMPELEKA VALERIE NYUMBANI**

- Irene (mke, 19)
- Valerie (mke, 19)
- Dora (mke, 18)
- Keshia (mume, 30)
- Msimulizi

#### **SCENE TWO: MALEMBA AWASILI JIJINI NYUMBANI KWA KALAMA**

- Malemba (mke, 35)
- Kalama (mume, 40)
- Msimulizi

## **SCENE THREE: KAPAKA NA MCHUNGAJI WARUDI NYUMBANI**

### **BAADA YA MATEMBEZI**

- **Mchungaji (mume, 40)**
- **Kapaka (mume, 25)**
- **Cheupe (mke, 25)**

### **UTANGULIZI:**

Nawasalimu na karibuni katika kipindi chetu **cha Noa bongo, Jenga maisha yako**. Hiki ni kipindi cha sita katika hadithi ya "**Bado ningali mwanadamu**". Kipindi kilichotupa kisogo, Malemba alimuomba Mizanja amsaidie nauli ya kumpeleka kijana wake Chumba jijini. Majirani zake hawakuwa na la mswalie mtume walipomchomea nyumba yake, sababu kuu ikiwa ni uchawi. Kwengineko, Kapaka hatimae alikubali kuwa na matembezi na mchungaji wake, baada ya binti yake kuzaliwa. Na Irene nae baada ya kujivinjari diskoni usiku uliopita na rafikiye Dora, wanafunzi hawa wa unesi walikutana na mwenzao Valerie: akiwa ameketi njiani uchi wa mnyama. Sasa tuanzie wapi? Hebu pata kuvutika na kunatika papo hapo ukitega sikio katika kipindi hiki cha leo kiitwacho, "**Hakuna jambo rahisi**". Tunaendelea palepale tulipokomea, wakati Irene na Dora walipokutana ana kwa ana na Valerie .

## **SCENE ONE: DORA NA IRENE WAMPELEKA VALERIE NYUMBANI**

**1. ATMO:                   NIGHT LIFE AMBIENCE IN THE STREETS**

**2. IRENE:                   (utterly shocked) Siamini macho yangu! Huyu kweli ni Valerie, mbona kabadilika hivi? Mbona yuko uchi, mchafu, na baridi hii kwenye njia hizi**

hatari? Dora, ni muhimu tumsaidie.

- 3. DORA:** Kivipi? Pia wewe umeshikwa wazimu? Irene, rafiki yako ni mwendawazimu, utamsaidiaje? Kama wendawazimu wanaweza saidika, basi wote wangelikuwa wameondoka kwenye miji. Hebu twende zetu. Wachana nae, usiku unazidi kuwa mwingi.
- 4. IRENE:** La, siwezi kumuacha Valerie apigwe na baridi jinsi hii, si haki. Mbali na hivyo, hapa amezingirwa na wahuni wa kila aina, wanaweza hata kumnajisi...
- 5. DORA:** Bila shaka, nafahamu hayo yote Irene. Lakini mambo hayo ni kawaida kwa wendawazimu. Tufanye hima, tuondoke tukapate angalau lepe la usingizi. Kumbuka, kesho tunadamkia darasani.
- 6. IRENE:** Wewe endelea... ninaangalia la kufanya. Kwanza nipatie hicho kitambaa chako, tunahitaji kumfunika angalau kidogo.
- 7. DORA:** Sahau! Kitambaa changu cha hariri hiki hakifungiwi mwendawazimu yeyote. Nililetewa zawadi mwenzangu. Samahani hilo sitalifanya.
- 8. IRENE:** Dora, nikifikiria kama wanafunzi wa uuguzi tunahitaji kuhurumia wagonjwa kwanza. Valerie anahitaji msaada wetu.

- 9. DORA:** Valerie anakuhitaji wewe! Mimi simo katika shimo... tuonane kesho chuoni.
- 10.SFX:** **HIGH HEELS TIP TOE INTO DISTANCE**
- 11. VALERIE:** **(shivering from cold)**
- 12. IRENE:** **(softly)** Valerie. unanikumbuka? Mimi nilikuwa...
- 13. VALERIE:** Irene... nahisi baridi.. niko baridi...
- 14. IRENE:** **(shocked)** Unanikumbuka? Kivipi? Ziko wapi nguo zako, Val? Ulikuwa wapi? Hebu tuondoke hapa kwanza.
- 15. VALERIE:** Irene... nahisi njaa... sijakula kitu...
- 16. IRENE:** Mbona unanibumbuwazisha! Unazungumza kama mtu mwenye akili timamu! Lakini si neno... vaa hili korti, najua halitakuzuia baridi lakini litakufikisha nyumbani salama.
- 17. MSIMULIZI:** Maradhi ya akili ni mengi na sio rahisi mtu kuyaelewa yote. Mengine hata wataalamu wa maradhi haya hushindwa kueleza chanzo chake. Ni kama tulivyomuona Valerie, kuugua wazimu hakukumaanisha kupoteza fahamu, au kuharibu fikra za mtu. Irene alifanya awezalo kumsitiri Valerie na nguo yoyote aliyoipata, na akatembea naye hadi kituo cha basi.

**18.ATMO:** **AT THE BUS STOP (AT NIGHT)**

**19.IRENE:** Valerie, sasa, tupande hili gari la abiria  
lilosimama. Halina watu ndani kwa hivyo, tutaketi  
kule nyuma peke yetu.

**20.SFX:** **SLIDING DOOR OF A VAN OPENING**

**21.ATMO:** **ENGINE RUNS AS THEY ENTER THE BUS**

**22.MTOZA NAULI:** **(arrogantly)** Eh, eh, wewe ! mnakwenda wapi?  
Hebu shukeni haraka, shuka chini, hili gari  
halibebi wendawazimu.

**23.IRENE:** Ati nini? Una akili kweli wewe? Ati umetuita sisi  
wendawazimu? Tafadhali chunga mdomo wako.  
Sisi pia tuna haki ya kusafiria basi hili. Rafiki  
yangu ni mgonjwa haja yangu ni kumpeleka  
nyumbani.

**24.MTOZA NAULI:** Bibiye... nimekueleza kuwa hatubebi  
wendawazimu. Ita teksi au gari ya wagonjwa.  
Shuka!

**25.IRENE:** Hii si haki. Acha nizungumze na dereva!

**26.MTOZA NAULI:** Mimi ndiye dereva, na mimi ni mpiga debe na

pia mwenye gari vilevile, kwa hivyo,  
tusipotezeane muda, shukeni mtafute usafiri  
mwengine.

**27.IRENE:** Sawa, nitalipia viti vyote vyta huko nyuma.

Turuhusu twende. Rafiki yangu anahitaji  
angalau kitu ale na hapa kuna baridi kali.

**28.MTOZA NAULI:** Sina haja na pesa zako, hunielewi? Nitakacho  
ni nyinyi muondoke garini mwangu! Unaona  
sasa: abiria wote wanaliepuka gari letu! Halafu  
kashaleta harufu mbaya hapa, hebu shukeni.

**29.SFX:** **HOOTING AND HONKING**

**30.IRENE:** Pole, Valerie, itatubidi tushuke.

**31.VALERIE:** **(suddenly scared)** Wanani fuata tena! La...sitaki  
kwenda!!

**32.IRENE:** Val, tafadhali usianze tena sasa, nakusihii.  
Tushuke halafu tutafute njia ya kurudi nyumbani.  
Sawa?

**33.VALERIE:** **(begging)** Nawaomba tafadhali msinichukue.  
Tafadhali usimchukue rafiki yangu Irene.

**34. IRENE:** Valerie, hakuna atakayethubutu kunichukua mimi  
au wewe popote, niko na wewe hapa. Haya  
tushuke!

**35. SFX:** **ENGINE SOUND fade out as they leave the van,**  
**BUS STOP ATMO gets louder again.**

**36. VALERIE:** **(fearful)** Siwezi kukaa hapa, watanichukuwa.

**37. IRENE:** **(screams, to conductor)** Tafadhali nisaidie  
nimzuie! Anataka kutoroka... msimamishe!

**38. MTOZA NAULI:** Ati nini? Hapana! Wazimu wenu pelekeni huko.

**39. SFX:** **FOOTSTEPS RUNNING AWAY INTO THE DISTANCE**

**40. IRENE:** **(shouting)** Valerie, rudi! Valerie, subiri!

**41. SFX:** **HIGH HEELS RUNNING INTO THE DISTANCE**

**42. MTOZA NAULI:** Siku ya leo ishaingia mkosi. Wanawake wawili  
wendawazimu wanafukuzana barabarani, leo  
bila shaka nishaingia hasara.

**43. MSIMULIZI:** Huwezi kuamini kuwa wenye maradhi ya akili  
huwa hawachukuliwi kama watu wa kawaida, lakini wanasumbuliwa  
kama wanyama. Ni kama ambao jamii inasema: haitambui kuwa

wanaishi. Irene anamfukuza akitaka kumkamata Valerie ambae anaogpa sauti za watu asioweza kuwaona na anakimbia. Lakini kwa sababu ya viatu vya visigino virefu alivyovaa Irene inakuwa ngumu kumfikia Valerie. Huku Irene akihema Valerie alipotelea gizani akiwa hana kitu kingine chochote isipokuwa korti la, rafiki yake, Irene. Siku hiyo hiyo katika jiji hilo, Malemba anawasili na kijana wake, Chumba, baada ya safari ya masafa mrefu. Sasa yuko mkabala na kakake mkubwa Kalama.

**SCENE TWO: MALEMBA AWASILI JIJINI NYUMBANI KWA  
KALAMA**

**44.SFX:**                   **KNOCKING ON DOOR**

**45.KALAMA:**           Ni nani?

**46.MALEMBA:**          Kalama ni mimi, Malemba.

**47.SFX:**                   **DOOR BEING UNLOCKED**

**48.KALAMA:**           Malemba! Nafurahi kukuona! Unafanya nini hapa? Oh Chumba... umekuwa baba mzima!

**49.MALEMBA:**          Kaka hatukaribishwi ndani kwanza? Tumekuwa na safari ngumu.

**50.KALAMA:**           Bila shaka, karibuni. Tafadhalii ketini, Chumba karibu ukae hapo karibu na ukuta. Niwaandalie nini?

- 51. MALEMBA:** Sote hatujala. Tutahitaji kula chochote. Lakini kwanza nina ujumbe wako.
- 52. SFX:** **SOMETHING BANGING AGAINST WALL**
- 53. KALAMA:** (**shocked**) Oh jamani, Chumba! Usijigonge kichwa chako kwa ukuta. Malemba, mzuie asijipige! Majirani hawawezi kustahimili kelele hizi.
- 54. MALEMBA:** Ah, itabidi wazoee kelele hizo. Sababu tuna azma ya kuishi hapa kwa muda, kama itakuwa sawa kwako.
- 55. KALAMA:** Ati? Muishi hapa kwa muda? Hapa wapi?
- 56. MALEMBA:** Hapa kwako eti. Kalama, wewe ndiye kakangu wa pekee, niende wapi kwengine? Wewe humuhurumii Chumba. Itabidi nimfunge kamba... lakini si hivi sasa
- 57. KALAMA:** Uhmm... Malemba... Sidhani kama hilo ni wazo muafaka. Mbali na hayo, unapokuwa unapanga kukaa hapa kule kwako Vikwatani kutaangaliwa na nani?
- 58. MALEMBA:** Sina makao. Nyumba yangu ilichomwa.

Nasikia kiu imenikaba, hamna chochote tukanywa?

**59. KALAMA:** (shocked) Imechomwa! Malemba, unaniambia nini? Akili yako timamu kweli ? Au pia wewe unaelekea...

**60. MALEMBA:** Sielekei popote. Tutaishi hapa mpaka tujenge makao mengine. Nafikiri niliomba chai angalau ninywe ama? Chumba hajakula chochote tangu tutoke kijijini, utumbo wake umeshikana na mgongo kwa njaa, maskini akitembea huwa hajulikani yuwaenda au yuwarudi...

**61. KALAMA:** Ninachotaka kujua ni kuwa hata wewe umeanza kuugua... Sawa, yapo maji debe zima pale sebuleni...

**62. SFX:** **WATER BEING POURED INTO A GLASS**

**63. MALEMBA:** Majirani walinchomea nyumba yangu. Wao wanaamini kuwa mimi ni mchawi na nimemroga Chumba awe mgonjwa namna hii, na ndio chimbuko la mikosi yangu yote.

**64. KALAMA:** Lahaula! Ilikuwa hivyo, sasa wewe na Chumba mlinusurika vipi?

- 65. MALEMBA:** Ni hadithi ndefu, kakangu. Lakini kwanza nijibu. Twaweza kuishi hapa au la?
- 66. KALAMA:** Ah...nafikiri...mnaweza...lakini kwa siku chache. Chumba hastahili kuonekana ni sharti afichwe! Sijaeleza watu kama nina mtoto yejote wa ndugu yangu sampuli hii.
- 67. MALEMBA:** Ni sawa. Jambo muhimu ni kumuona daktari maalum wa matatizo yake. Lakini tutakwenda mapema kesho asubui.
- 68. SFX:** **RUSTLING OF NEWSPAPERS**
- 69. KALAMA:** (to Chumba) Enhe Chumba, mbona unayapanga hayo magazeti kwani unataka kuyafanyaje? Unajenga mnara wa magazeti?
- 70. MALEMBA:** Hivyo ndivyo anavyofanya akiwa nyumbani na mizigo ya kuni.
- 71. MSIMULIZI:** Chumba ana matatizo ya kupanga vitu kwa msururu kila wakati anapopata fursa hii. Lakini hali hii ya ugonjwa inatambulikaje? Tutajua hivi punde. Lakini kwanza turudi nyumbani kwa Kapaka. Bado anaugua yale maradhi yake ya “depression” kama wataalamu wasemavyo, na ndiyo amerudi sasa kutoka matembezi na mchungaji.

**SCENE THREE: KAPAKA NA MCHUNGAJI WANARUDI NYUMBANI**

## **BAADA YA MATEMBEZI**

**72.SFX:**                   **DOOR BEING UNLOCKED**

**73.MCHUNGAJI:**     Huo ulikuwa muda mwanana wa matembezi,  
ama unasemaje.

**74.CHEUPE:**         Afadhali mmerudi. Nilianza kuwa na wasiwasi...

**75.SFX:**                   **INFANT NOISES**

**76.CHEUPE:**         Natumai mlipata muda wa kuyazungumza?

**77.KAPAKA:**         La, hatukuzungumza chochote. Lakini  
tulipendezwa na sauti za ndege na sisimizi  
zilizotawala chakani. Nilikuwa kitambo sijawahi  
kusikia sauti hizo.

## **HITIMISHO:**

Hayo maneno fasaha kutoka kwa Kapaka baada ya muda mrefu tangu alipoanza kuugua, maradhi ya akili ya “depression” yanatufungia kipindi hiki cha sita katika makala yanayoendelea ya hadithi hii ya maradhi ya akili barani Afrika. Je, kulitokea nini? Iwe kwamba Kapaka amekwisha kupona? Kutatokea nini kwa Malemba na Chumba kule jijini? Je, Irene atampata Valerie tena? Kwa haya na mengineyo mengi, jiunge nasi katika kipindi kifuatachao. Ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki, tembelea wavuti wetu [www.dw.de/lbe](http://www.dw.de/lbe). Hadi wakati mwengine. Kwaheri.